# Uamilifu wa Jazanda Kwenye Nyimbo za Kiasili za Kikamba

**Elizabeth K. Mue, Magdaline N. Wafula & Robert Oduori**
*Moi University, Kenya*

**Uwasilishaji wa Makala**
*Pokelewa: 2024-04-22*
*Rekebishwa: 2024-08-02*
*Kubalika: 2024-08-23*
*Chapishwa: 2024-08-29*

***Maneno Muhimu***
Itikadi
Jazanda
Nyimbo
Uwanja Lengwa
Kikamba

**Jinsi ya Kurejelea Makala:**
Mue, E. K., Wafula, M. N. & Oduori, R. (2024). Uamilifu wa Jazanda Kwenye Nyimbo za Kiasili za Kikamba. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, 2(2), 25-33.

*Copyright © 2024*

**Ikisiri**
Jamii ya Wakamba huwasiliana kwa njia mbalimbali fasihi simulizi ikiwa njia mojawapo. Fasihi simulizi ya Wakamba hujumuisha vipera anuai nyimbo za kiasili zikiwemo. Nyimbo za kiasili ni maarufu na huwasilishwa katika takriban kila shughuli na hafla za kijamii. Kupitia nyimbo hizi, itikadi ya Wakamba huwasilishwa kwa hadhira. Hata hivyo, itikadi hii aghalabu hufumbatwa kijazanda. Makala haya yanatathmini uamilifu wa jazanda mahsusi kifani na kimaudhui kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba. Data ya utafiti imechanganuliwa na maelezo kutolewa kulingana na malengo ya utafiti na mihimili ya kinadharia. Nadharia ya Jazanda Dhanifu imeuongoza uhakiki wa data. Data ya kimsingi ilitokana na nyimbo za kiasili za Kikamba zilizokusanywa kutoka Tume ya *Permanent Presidential Music Commission* nchini Kenya. Nyimbo zilizosheheni jazanda zilisampuliwa kimakusudi. Matokeo ya utafiti huu ni rejeleo muhimu kwa taaluma ya fasihi simulizi ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika.

## Utangulizi

Makala haya yanachanganua uamilifu wa jazanda mahsusi kifani na kimaudhui katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Kwa mujibu wa King'ei na Kisovi (2005), fani ni ufundi wa kisanaa katika kazi ya fasihi. Ni mbinu za kiufundi zinazotumiwa na mtunzi kuwasilisha masuala fulani kupitia kwenye kazi yake ya fasihi. Kwa upande mwingine, King'ei na Kisovi (keshatajwa) wanayafafanua maudhui kama masuala makuu yanayojitokeza katika kazi ya fasihi. Kama anavyoeleza Senkoro (2011), fani na maudhui ni vipengee visivyoweza kutenganishwa. Hii ni kwa sababu vipengee hivi vinaingiliana na kukamilishana. Ni kama pande mbili za sarafu moja. Huku maudhui yakijibu swali la ni nini kinachowasilishwa, fani hujibu swali la ni vipi kinavyowasilishwa.

King'ei na Kisovi (2005) wanaeleza kwamba fasihi hutumia fani au ufundi fulani wa kimasimulizi ili kuwasilisha maudhui fulani kuambatana na matakwa ya mtunzi. Jazanda ni mojawapo ya vipengee vya fani katika fasihi. Kwa mujibu wa Syambo na Mazrui (1999), uchambuzi wa fasihi haukamiliki bila kutalii ujumbe wa msanii pamoja na mbinu za kisanaa anazotumia kuwasilisha ujumbe huo. Mbinu za kisanaa ni kama vile jazanda. Hivyo si rahisi kufahamu ujumbe wa utungo wa fasihi iwapo hatuelewi jazanda zilizooufumbata ujumbe unaohusika. Jazanda ni dhana ambayo imezungumziwa na wataalam mbalimbali. TUKI (2018), inafafanua jazanda kama picha inayomwingia mtu kichwani. Nowottny (1962) anasema kwamba, jazanda inaleta picha ambayo inatufanya kuona jambo zaidi ya maana yake halisi. Nowottny (keshatajwa) anadai kwamba, katika jazanda mtunzi husema kuhusu jambo X kana kwamba ni Y. Yaani, anatumia istilahi Y kurejelea X.

Kwa mujibu wa Kovecses (2002), jazanda ni mchakato wa kiakili ambapo uwanja mmoja wa ufahamu (B) unaeleweka kwa misingi ya uwanja mwingine (A). Hivyo, jazanda huwa na uwanja asilia (A) na uwanja lengwa (B) kwa namna ambavyo uwanja asilia unahusisha vitu vinavyoweza kuonekana na kushikika huku uwanja lengwa ukiaminika kuhusisha vitu dhahania kwa kiasi fulani. Kwa hivyo, jazanda ni mfumo wa lugha ya kiishara ambapo uhusiano usiokuwa wa moja kwa moja hufanyika kati ya vitu viwili tofauti vilivyo na mfanano fulani. Katika jazanda, kitengo fulani hueleweka kwa misingi ya kitengo kingine. Uchunguzi na uchanganuzi wa jazanda huhusishwa na mwanafalsafa wa Kigiriki Aristotle (383-K.K-322 K.K). Aristotle, akirejelewa na Lan Chun (2003), anaeleza kuwa jazanda ni 'kule kupatia kitu jina la kitu kingine, ambapo uhamishaji huo huhusisha sifa zenye mahusiano'. Naye Leech (1969) anasema kwamba, jazanda inahusishwa na kanuni mahususi ya uhamisho ambayo inaitwa 'kanuni ya jazanda'. Akizungumzia dhana hii, Richard I.A. (1936) anaeleza kwamba maelezo ya kijazanda katika lugha huwa ni dhana mbili katika moja. Hivyo, jazanda sio kitu cha kiisimu tu bali pia ni namna ya kufikiria.

Kulingana na Lakoff na Johnson (1980), jazanda ni kitu dhanifu kinachohusishwa na mienendo na fikra za watu. Kulingana nao, jazanda sio lugha tu, bali pia ni mchakato wa kufikiria. Kwa kuzingatia mtazamo wa Isimu Tambuzi, jazanda inaelezwa kama ufafanuzi wa uwanja dhanifu mmoja kwa kurejelea uwanja dhanifu mwingine. Akizungumzia dhana hii, Kovecses (2003), anaeleza kwamba ufasiri wa jazanda unahusisha kufafanua uwanja dhanifu lengwa (B) kwa kurejelea uwanja dhanifu asilia (A). Mtaalamu huyu anairejelea hii kama jazanda dhanifu. Kwa mujibu wa Mbatia (2000), jazanda ni kunga ya utunzi ambapo lugha inatumiwa kusawiri picha fulani kutokana na maelezo yanayotumia maneno teule au tamathali za usemi. Kwa njia hii, mtunzi anamwezesha msomaji kuona, kuhisi au kunusa kitu kinachoelezwa. Naye Honara na mwenzake (2012) wanaeleza kuwa jazanda ni za aina tatu kuu: kiubia, jamii na za kibinafsia. Okwena (2013), ameainisha jazanda kulingana na rangi, wanyama, mimea, miti, ndege, ndoto, harufu na kadhalika.

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), jazanda hutekeleza dhima mahsusi kifani kuhusiana na kile kinawasilishwa kwa hadhira. Mbali na kufumbata itikadi kama kipengee mojawapo cha maudhui katika nyimbo za kiasili za Kikamba, jazanda hutekeleza dhima mahsusi kifani kuhusiana na kile kinawasilishwa. Hii ni athari ambayo humpata msikilizaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba ambamo jazanda hutumika. Utafiti huu umetambua kwamba jazanda hutekeleza dhima mbalimbali kifani na kimaudhui katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Kovecses, Z. (2002) anaeleza kwamba, neno linatumika kijazanda ili kupata urembo fulani wa kusema. Kwa mfano, jazanda huchangia katika kuchora taswira zinazorahisisha uelewa wa ujumbe katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Jazanda pia hukuza na kutanua maana ya dhana. Vilevile, jazanda huimarisha kumbukumbu ya itikadi zinazowasilishwa, huimarisha ujumi wa lugha na kukuza hisia za hadhira. Pia, jazanda husafidi lugha katika nyimbo za kiasili za kikamba, huzua utata wa kimaana kwa nia ya kuitenga hadhira lengwa pamoja na kukuza fikra za kiuhakiki miongoni mwa hadhira.

**Msingi wa Kinadharia**

Makala haya yamejikita kwenye nadharia ya Jazanda Dhanifu. Nadharia yenyewe inaichukulia jazanda kuwa kipengee muhimu cha lugha na ambacho hutekeleza kazi maalum katika matini za fasihi. Nadharia hiyo imeasisiwa na kuendelezwa na wataalam mbalimbali. Kwa mujibu wa utafiti huu, tumezingatia mkabala wa Lakoff na Johnson (1993). Mtazamo huu unajihusisha na ufasiri wa jazanda. Waasisi hawa wanashikilia kwamba ufasiri wa jazanda unahusisha kufafanua uwanja dhanifu lengwa (B) kwa kurejelea uwanja dhanifu asilia (A). Yaani, dhana moja inafafanuliwa kwa misingi ya dhana nyingine.

***Mihimili ya Nadharia ya Jazanda Dhanifu***

Nadharia hii ina misingi mitatu ifuatayo:

***i). Ukawaida wa Jazanda***

Mhimili huu unashikilia kwamba jazanda hutumika kwa njia mbalimbali ambapo matumizi yake huzoeleka na watumiaji wa lugha inayohusika. Uzoefu wa maelezo ya kijazanda huimarisha maana za kimsingi katika akili za wazungumzaji wa lugha yoyote inayohusika. Kwa mfano, katika wimbo *Kwa Sisya Wone* (Angalia Uone) ubeti wa 1, neno *mbilano* (kazi) limezoeleka kama linalotumika kijazanda kurejelea ngono kwenye muktadha husika. Jazanda hii imetumika kuwasilisha ujumbe kuhusu itikadi ya tohara kwamba ndicho kivukio cha kutoka utotoni hadi utu uzima. Baada ya kupashwa tohara, wahusika wana idhini ya kuoa na kushiriki ngono ambalo ni tendo la kuiendeleza jamii. Matumizi ya jazanda *mbilano* (kazi) yanaweza kusababisha utata wa kimaana kwa nia ya kuitenga hadhira. Hivyo, dhana ya ngono inakusudiwa ieleweke tu na watahiriwa na watu wazima pekee. Watoto wametengwa hapa ambapo watabaki kuishikilia maana ya kijuu juu.

***ii). Umbo Dhanifu la Jazanda***

Mhimili huu unashikilia kwamba jazanda ni tukio la lugha linalotumia dhana ili kuwasilisha dhana nyingine. Katika kuzifasiri jazanda, mfasiri anahamisha sifa za Uwanja asilia (A) anaoufahamu, hadi katika Uwanja lengwa (B) asioufahamu, ili kuelewa maana iliyokusudiwa. Kwa mfano, katika wimbo *Munuve*, dhana *simba wenye kucha* limetumika kijazanda kurejelea *viongozi fisadi* wanaotumia mamlaka yao vibaya. Jazanda hii inaibua taswira na hisia ya uoni. Taswira yenyewe inathabitisha itikadi kuhusiana na siasa na uongozi kwamba watu fisadi hawastahili kupewa wadhifa wa uongozi. Jazanda hii inaweza kuiathiri hadhira kichanya kwa kuifanya iwe makini katika harakati za kuchagua viongozi.

***iii). Uhusishaji wa Jazanda na Tajriba halisi za Wazungumzaji wa Lugha katika Mazingira husika***

Mhimili huu unaeleza kwamba ufasiri wa jazanda unahusisha kuelewa uzoefu halisi wa mtumiaji wa lugha. Uundaji, ufasiri na uelewekaji wa jazanda huhusisha mchakato wa kiutambuzi pamoja na uhamishaji wa maana kwa mujibu wa maarifa ya kimsingi yanayohusiana na mazingira yake. Kwa mfano, kupitia kwa wimbo *Usumbi ni Nzou* (Urais ni Ndovu) ubeti wa 1, neno *nzou* (ndovu) limezoeleka kama linalotumika kijazanda kurejelea urais. Haya ni kulingana na mazingira ya uwasilishaji wa wimbo huu. Msikilizaji wa wimbo anapoisikia jazanda hiyo, sifa au picha ya ndovu akilini mwake inahamishwa kwenye dhana ya urais na hivyo kuimarisha kumbukumbu kuhusiana na dhana ya urais. Jazanda hii pia inathabitisha ujumbe kuhusiana na wadhifa wa urais kwamba ni mzito na kwa hivyo, unahitaji umakinifu na nguvu kuutekeleza.

**Mbinu za Ukusanyaji na Uwasilishaji wa Data**

Makala haya yanatokana na utafiti wa uzamifu wa mtafiti unaohusu ufumbaji wa itikadi kijazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba. Utafiti wenyewe ni wa mkabala wa kimaelezo kwenye uwanda wa kithamanio. Mkabala huu umempa mtafiti nafasi ya kutoa ufafanuzi na maelezo mwafaka kuhusiana na data na matokeo ya utafiti. Kwa mujibu wa makala haya, nyimbo 12 ziliteuliwa kimaksudi kati ya nyimbo 100 zilizokusanywa kwenye tume ya *Permanent Presidential Music Commission* nchini Kenya. Uteuzi wenyewe ulifanywa kulingana na malengo na nadharia za utafiti. Data iliyokusanywa ilipangwa na kuchanganuliwa kwa kuiainisha kulingana na lengo. Uchanganuzi na ufasiri wa data umeongozwa na lengo na mihimili ya nadharia ya Jazanda Dhanifu. Baada ya uchanganuzi na ufasiri wa data, upangaji na uwasilishaji wa matokeo umefanywa kwa njia ya kimaelezo.

Vol. 2 No. 2 (2024): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v2i2.686


**Matokeo ya Utafiti**

Katika sehemu hii tumeangazia matokeo kwa mujibu wa lengo la utafiti. Tumejihusisha na uamilifu wa jazanda kifani na kimaudhui katika Nyimbo za kiasili za Kikamba.

**Jazanda katika kukuza na kuwasilisha maana**

Utafiti huu umetambua kwamba jazanda huwasilisha maana fulani. Kwa mujibu wa nadharia ya Jazanda Dhanifu, maana inayowasilishwa na jazanda huunda uhusiano fulani kati ya uwanja lengwa na uwanja asilia katika akili ya hadhira. Kwa hivyo, hali hii ndiyo humpa msikilizaji au mtazamaji wa wimbo wa kiasili mtazamo unaohusiana na itikadi inayowasilishwa. Mbinu hii ya kifasihi ya jazanda huipa nguvu lugha ya kishairi na uimbaji. Hili hufanyika kwa kuyakuza mawazo pamoja na kuendeleza uelewa wa msikilizaji wa ujumbe kwenye wimbo unaohusika. Kwa njia hii, jazanda hurahisisha ufasiri wa ujumbe kama vile kuchora taswira zinazoeleweka na hadhira. Taswira hizo huhusisha mambo magumu na yale yaliyo rahisi kueleweka. Kwa mfano, jazanda ya *ng'ombe sya mutavo* inajitokeza kwenye wimbo *Muvisi Ungi* (Kijana Mwingine), ubeti wa kwanza . Tazama mshororo ufuatao:

> ***Ng'ombe sya mutavo*** *syendaa na ungi*
> ***Ng'ombe wa wizi*** *hutoroshwa kwa wizi pia*

Neno ng'ombe wa wizi limetumika kijazanda kurejelea mali ya wizi. Jazanda yenyewe inalinganisha sifa za ng'ombe wa wizi na zile za mali ya wizi. Hapa, ng'ombe wa wizi (mnyama) ndio uwanja asilia huku mali ya wizi (Wanyama na vitu vinginevyo) ikiwa uwanja lengwa. Kutokana na uchanganuzi huu, upo mfanano kati ya ng'ombe wa wizi na mali ya wizi. Mfanano wenyewe ni kwamba yote ni mali inayopatikana kwa njia ya ufisadi na pia haiwanufaishi wahusika wanaoiiba. Hivyo, jazanda hii imetumika kuwasilisha itikadi ya jamii kuhusu ufisadi. Kupitia kwenye jazanda hii, mwimbaji anawasilisha mtazamo hasi kuhusiana na ufisadi kwamba haufai kitu kwa maana hauna manufaa yoyote. Hapa, mwimbaji anaieleza umma kuhusu madhara yanayosababishwa na ufisadi. Kutokana na maarifa ya kimsingi kwenye akili ya mfasiri, msikilizaji anaifasiri jazanda yenyewe kwa kutambua sifa zifuatazo:

| **Ng'ombe wa Wizi (Uwanja asilia A)** | **Mali ya Wizi/ufisadi (Uwanja lengwa B)** |
|---|---|
| Ni wanyama | Huhusisha wanyama na vitu vinginevyo pia |
| Hupatikana kwa wizi/ufisadi | Hupatikana kwa wizi/ufisadi |
| Hupotea kwa njia hiyo ya wizi tu | Hupotea kwa njia hiyo ya wizi tu |
| Haimnufaishi mhusika | Haimnufaishi mhusika |

Kutokana na kifungu kilichopo hapo juu, dhima ya jazanda ni kukuza maana kuwa wizi na ufisadi ni mienendo isiyofaa miongoni mwa wanajamii.

**Jazanda Huimarisha kumbukumbu na kuthabitisha Ujumbe**

Jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba zimetumiwa kukuza na kuthabitisha ujumbe unaowasilishwa na pia kuimarisha kumbukumbu ya hadhira. Hali hii inadhihirika katika jazanda ya *usumbi* (urais) kwenye wimbo *Usumbi ni Nzou* (Urais ni Ndovu), kifingu cha kwanza. Katika jazanda hiyo, wadhifa wa urais unalinganishwa na ndovu. Msikilizaji wa wimbo anapoisikia jazanda hiyo, sifa za ndovu au picha ya ndovu akilini mwake inahamishwa kwenye dhana ya urais na hivyo kuimarisha kumbukumbu kuhusiana na dhana ya urais. Jazanda hii pia inathabitisha ujumbe kuhusiana na wadhifa wa urais kwamba ni mzito na kwa hivyo, unahitaji umakinifu na nguvu kuutekeleza.

Mfano mwingine wa jazanda yenye uamilifu wa aina hii ni *ngima* (ugali) inayopatikana kwenye wimbo *Kavuli Vula Mwee Witu*. Tazama mshororo ufuatao:

> ***Ngima** yumaa kwi kuthie*
> **Ugali** hupatikana kwa kusiaga.

Neno ugali limetumika kijazanda kurejelea mafanikio. Jazanda hii inafumbata itikadi kuhusu kazi kwamba ***mafanikio*** hupatikana baada ya kujitahidi kazini. Hapa, sifa na picha ya ugali iliyo kwenye akili ya msikilizaji inahamishwa kwenye dhana ya mafanikio ambapo kumbukumbu ya dhana hiyo inaimarishwa. Jazanda ya **Ngima** (**ugali**) pia inathabitisha ujumbe kwamba mafanikio hupatikana baada ya kujitahidi kazini. Hivyo, jazanda ya **ugali** inawasilisha itikadi kuhusu kazi kwamba wanajamii hawana budi kutia bidii kazini ndiposa wafanikiwe.

**Jazanda Huimarisha ujumi wa Lugha**
Matumizi ya jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba huzua urembo fulani wa kisanaa katika lugha. Matumizi ya jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba huzifanya zipendeze masikioni mwa hadhira na kwa hivyo kuvuta makini ya hadhira kwenye ujumbe unaowasilishwa. Tazama mshororo huu unaopatikana katika wimbo *Kavuli Vula Mwee witu*:

> ***Kavuli** vula mwee witu.*
> **Kavuli** twanga mawele yetu.

Katika mshororo uliopo hapo juu, jina K**avuli** limetumiwa kijazanda na kimajazi kurejelea mtu mwenye bidii kazini. Zaidi ya hayo, jazanda hiyo katika lugha ya Kikamba inaleta wizani na ladha fulani ya kishairi kupitia kwa maneno ***Kavuli vula*** (mtwangaji twanga). Hapa kuna takriri ya mizani **vu-li** na **vu-la** ambayo inavutia masikioni na kuimarisha burudani ya hadhira.

Dhima ya ujumi wa lugha inadhihirika pia katika mshororo ufuatao wa wimbo *Mutanu*:

> *Nauma kwasa nayu ningwenda **katanda** ngome*
> Nimetoka mbali na sasa nataka **kitanda** nilale.

Katika mshororo uliopo hapo juu, neno kitanda limetumika kijazanda kuashiria ndoa. Kauli ya kutoka mbali inarejelea mhusika aliyekomaa kihulka na kitanda ni jazanda ya ndoa. Itikadi inayowasilishwa hapa inahusu ndoa kwamba ni ya wale wamekomaa kiakili na kimwili. Jazanda hizi zinachochea taharuki katika hadhira na kwa njia hii kuifanya itafakari kwa kina kutafuta fasiri ya ujumbe uliofumbatwa na jazanda hizo. Hapa, lugha ya kimafumbo inazua ladha ya kisanaa kwenye wimbo wa kiasili.

**Jazanda hujenga Taswira mbalimbali**
Kwa mujibu wa Wamitila (2003), taswira ni maneno ambayo hujenga hali au picha fulani kwenye akili ya hadhira. Taswira zenyewe zinaweza kugawanyika katika aina mbalimbali. Aina hizi ni kama vile taswira hisi, taswira ya mawazo, taswira muonjo na taswira mnuso miongoni mwa nyingine. Matumizi ya jazanda huathiri hisia za hadhira kuhusiana na masuala yanayowasilishwa katika nyimbo za kiasili za Kikamba. Matumizi ya jazanda huibua picha akilini mwa hadhira na kwa njia hii hufanya suala linalowasilishwa lieleweke kwa urahisi. Kupitia kwa jazanda msikilizaji au mtazamaji wa nyimbo hizi huhusisha vitu vinavyolinganishwa ambapo hatimaye huunda picha akilini. Kwa mfano angalia mshororo huu:

> ***Simba ii syi ngunyu** nitwasyelile.*
> ***Simba wenye kucha** tushazikatakata*

Hapa, neno simba wenye kucha limetumika kijazanda kurejelea *mienendo ya wanasiasa fisadi*. Mwimbaji anatumia jazanda ya ***simba wenye kucha*** kurejelea viongozi ambao wametumia mamlaka yao vibaya na ambao wameshatupiliwa mbali na wapiga kura. Msikilizaji anahusisha picha ya simba wenye kucha na viongozi fisadi ambao hawastahili kupewa wadhifa wa uongozi. Jazanda hiyo inaibua taswira na hisia ya uoni ambayo inathabitisha mielekeo kuhusu siasa na uongozi katika jamii ya Wakamba. Watu fisadi hawastahili kupewa wadhifa wa uongozi. Jazanda hii inaweza kuiathiri hadhira kichanya kwa kuifanya iwe makini katika harakati za kuchagua viongozi. Jazanda yenyewe inadhihirika katika wimbo *Munuve*.

**Jazanda Husababisha utata wa Kimaana kwa madhumuni ya Kuitenga Hadhira Lengwa**

Wakati mwingine, uwepo wa jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba unaweza kusababisha utata wa kimaana wa ujumbe unaowasilishwa. Hali hii inamsaidia mwimbaji katika kuitenga hadhira yake. Hivyo, ujumbe hueleweka tu na wale waliokusudiwa. Hii ni kwa sababu mwimbaji anaweza kuficha maana kamili za maneno katika jazanda husika. Hivyo, maana za jazanda zinaweza tu kueleweka na hadhira maalum kutokana na msingi fulani wa maarifa walio nayo. Hivyo, uelewekaji wa jazanda inayohusika hutegemea uzoefu na mazingira ya mwimbaji na hadhira. Tazama mfano ufuatao wa jazanda kutoka kwa wimbo ***Kwa sisya Wone*** (***Angalia Uone***):

> ***Muti uu ni mumu***
> Mti huu umekauka/umekomaa

Kwenye mfano huo, maneno *mti uliokauka/uliokomaa* yametumika kijazanda kurejelea mboo za watahiriwa. Maana ya jazanda hii inaweza kueleweka vyema na hadhira inayoufahamu muktadha wa tohara katika jamii ya Wakamba. Mboo za watahiriwa zinalinganishwa na mti uliokomaa kumaanisha kuwa watahiriwa wana idhini ya kushiriki ngono pindi tu wanapopata jiko. Hata hivyo, mwanajamii asiyeufahamu muktadha ambamo jazanda hii inatumika huenda akatatizika. Kwa mfano, vijana wadogo ambao hawajatahiri wametengwa katika muktdha huo. Hii ni kwa sababu ujumbe wenyewe umewalenga watahiriwa pekee.

Mfano mwingine wa jazanda inayosababisha utata wa kimaana kwa madhumuni ya kuitenga hadhira lengwa upo kwenye mshororo huu:

> *Syana syokote* ***malenge*** *kivulanio kya* ***nzuu*** *na* ***mboso****.*
> Watoto waokote **maboga**, mchanganyiko wa **baazi** na **maharagwe**.

Katika wimbo *Tuthii Kithembeoni* (Twendeni Madhabahuni) tunapata maneno ***Malenge*** (Maboga), *Nzuu* **(**Mbaazi**)** na *Mboso* **(**Maharagwe**)** ambayo yametumika kijazanda kurejelea dhana ya mafanikio yanayotokana na kumwabudu Mungu. Hivyo, hali hii ya dhana nyingi kurejelea dhana moja pia ni utata wa kimaana. Hata hivyo, hadhira lengwa haina budi kuuelewa ujumbe unaowasilishwa. Hii ni kutokana na uelewa wa muktadha wa uimbaji wa wimbo unaohusika.

Vilevile, maana ya jazanda ya **ndovu** katika wimbo *Usumbi ni* ***Nzou*** (Urais ni **Ndovu**) na wimbo *Ngai wa* ***Nzou*** *nowe wa* ***Nduti*** (Mungu wa **ndovu** ndiye Mungu wa **siafu**) ni tofauti. Neno **ndovu** kwenye wimbo *Usumbi ni* ***Nzou*** limetumika kurejelea cheo cha **urais** huku neno hilo hilo likitumika kurejelea **tabaka tawala** katika wimbo *Ngai wa* ***Nzou*** *nowe wa* ***Nduti.***

Angalia kauli hizi:

> *Usumbi aume ni* ***nzou****.*
> Jamani urais ni **ndovu**.

*Ngai wa **nduti** nowe wa **nzou**.*
Mungu wa **siafu** ndiye wa **ndovu**.

Katika mifano hiyo yote, neno **ndovu** linazua utata wa kimaana kwa nia ya kuitenga hadhira lengwa. Hii ni kwa sababu neno hilo linaweza kutumika katika kuwasilisha maana tofautitofauti kutegemea muktadha wa wimbo unaowasilishwa. Mbali na kuzua utata kimaana, jazanda kama kipengee cha fani inakuza tafakuri ya hadhira katika kufumbua maana fiche. Maana hii fiche ndiyo itikadi maalum inayowasilishwa kisanaa.

**Jazanda Hukuza Fikra za Kiuhakiki**
Uwepo wa jazanda katika nyimbo za kiasili za Kikamba unaweza kumfanya msikilizaji au mtazamaji atafakari zaidi kuhusiana na wimbo unaohusika. Hivyo, matumizi ya jazanda katika nyimbo zinazohusika yanaweza kukuza mijadala na uhakiki wa dhana maalum, hali inayoweza kuibua mtazamo mbadala kuhusu dhana ambazo kidesturi zimechukuliwa kuwa na maana moja maalum. Kwa maneno mengine, jazanda huchangia katika udenguzi wa maana katika dhana na masuala yanayowasilishwa kwenye wimbo wa kiasili. Kutegemea muktadha ambamo nyimbo za kiasili zinawasilishwa, jazanda zilizomo zinaweza kufasiriwa kwa njia mbalimbali. Hivyo, msikilizaji husikiliza au kuutazama wimbo unaohusika kwa njia ya kiuhakiki. Uhakiki wenyewe hutokana na hali ya kuutafuta ukweli uliofichika katika jazanda na itikadi zinazowasilishwa kupitia nyimbo zinazohusika. Kwa mfano, katika wimbo *Sikala* tunapata jazanda ya *sikala* (sigara). Katika wimbo huu, tunaelezwa namna ambavyo mwimbaji amemwomba msichana Manguleti sigara bila mafanikio. Neno *sigara* limetumika kijazanda kurejelea *ngono*. Tukio la Manguleti kumnyima mwenzake *sigara* limetumika kuwasilisha itikadi ya jamii kuhusu ubikira kwamba ni jambo muhimu na la kuzingatiwa na vijana hasa wa kike. Kabla ya kufikia ufasiri huu wa jazanda teule, msikilizaji hana budi kufikiria kiuhakiki ndiposa aweze kupata maana iliyokusudiwa. Hapa unajiuliza je, sigara inaashiria nini, ina uhusiano upi na ujumbe unaowasilishwa na pia je, ni nini hasa kinachohitajika kutoka kwa mhusika wa kike Manguleti?

**Jazanda Hupanua maana ya Dhana**
Jazanda hutumika katika kupanua dhana fulani kwa kuifafanua zaidi. Wahusika na wasikilizaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba huzingatia zaidi kinacholinganishwa katika wimbo husika. Kwa mfano, jazanda ya *mutunda* (mtunda) inajitokeza kwenye wimbo *Nzambi wa Mutunga.* Angalia mshororo huu:

*Mbande **mutunda**, ni waki? Wai wa mavatano.*
Nipande **mtunda**, ni wa nini? Ulikuwa wa mapatano.

Kutokana na mfano huo, dhana ya ***Mtunda*** inarejelea mapatano/makubaliano kati ya wanandoa. Kupitia matumizi ya jazanda hii, dhana ya mtunda imepanuliwa kimaana na kimatumizi. Hii ni kwa sababu unaweza kutumia dhana hizi mbili ***mtunda*** na mapatano kurejelea kitu kimoja. Hivyo, dhana inayowasilishwa hapa imekuzwa na kupanuliwa kwa kupewa maana nyingine.

Mfano mwingine ni ufuatao:

***Munyambu** nuukiva*
**Simba** ananguruma

Jazanda ya *simba* inadhihirika katika wimbo *Munyambu Nuukiva*. Jazanda yenyewe inarejelea ngariba katika muktadha wa tohara. Kwa msingi huu, matumizi ya jazanda ya ngariba imepanuka kiupeo wa kimatumizi. Hivyo, mzungumzaji anaweza kutumia istilahi zote mbili; ***ngariba*** na ***simba*** kurejelea kitu kimoja.

**Jazanda na Uashiriaji**

Kutokana na ukweli kwamba jazanda ni ulinganishaji, uwanja mmoja huwa ishara ya mwingine. Tunapolinganisha A na B, uwanja B huwasilisha sifa au dhima za uwanja A. Kwa hivyo, jazanda zote zinatekeleza dhima ya uashiriaji. Kwa mfano, katika wimbo *Muika Wia Nukunwe* tunapata jazanda ya ndeke (ndege). Tazama mshororo ufuatao:

*Ve **ndeke** ikwitwa Manyali ikakua andu ma wia*
Kuna **ndege** inaitwa Manyali itabeba watu wa kazi

Mfano huu unabainisha jazanda ya ndege ambayo inaashiria mafanikio. Hivyo, sifa ya kupaa juu kwa ndege inalinganishwa na mafanikio ambayo ni kufikia kiwango cha juu kimaendeleo. Kwa hivyo, mwimbaji anapotaja kwamba *ndege Manyali* itabeba watu wa kazi anaashiria kwamba mafanikio hupatikana kwa watu walio na bidii kazini. Kwa hivyo, jazanda yenyewe inafumbata itikadi kwamba ni sharti mtu afanye kazi kwa bidii maishani ili kupata mafanikio.

**Jazanda hutumika kama Tasfida**

Mwimbaji wa nyimbo za kiasili za Kikamba anaweza kutumia jazanda kurejelea dhana fulani ambazo ni mwiko kuzitaja moja kwa moja. Kwa mfano, jazanda hutumiwa kurejelea mielekeo maalum ya kisiasa, magonjwa sugu pamoja na sehemu nyeti za mwili. Kwa mfano, katika wimbo *Nzambi akithambya **Nzele** (Nzambi akiosha **kata**)*, tunapata jazanda hii:

***Nzambi** akithambya nzele ii ya kuthamba.*
***Nzambi** akiosha **kata** ya kuoga.*

Hapa, mwimbaji anaitumia jazanda ya uoshwaji wa ***nzele*** kurejelea uondoaji wa uozo wa kijamii unaotekelezwa na viongozi watangulizi. Hapa suala la ufisadi wa viongozi ni suala nyeti ambalo wanajamii huogopa kulieleza moja kwa moja hasa katika harakati za kampeni za kutafuta kura. Kwa hivyo, kutokana na hali hii, mwimbaji hana budi kutumia lugha ya kijazanda ili kupunguza makali ya ujumbe wake kwa hadhira ili itafakari juu ya wale wanastahili kupewa fursa ya uongozi. Kwa kufanya hivi, mwimbaji huuimba wimbo wake kama fumbo linalohitaji kufumbuliwa ndiposa itikadi zinazowasilishwa zipate kueleweka.

Mfano mwingine wa jazanda zinatumika kusafidi lugha ni huu ufuatao:
*Ala matesi **mbilano***
Wasiojua ***kazi***

Neno ***mbilano (kazi)*** limetumika kijazanda**.** Jazanda yenyewe inajitokeza katika wimbo *Kwa Sisya Wone* (**Angalia Uone**). Hapa, mwimbaji anaitumia jazanda ya *mbilano* kuashiria n*gono.* Neno mbilano (kazi) ni tasfida inayopunguza makali kihisia na kuepuka aibu ambayo ingezuliwa iwapo maneno halisi yanayorejelea dhana hiyo yangetumiwa. Kwa hivyo jazanda ni kipengele muhimu cha kusafisha lugha zikiwemo nyimbo za kiasili za Kikamba zinazowasilishwa katika hafla mbalimbali za kijamii.

Pia, katika wimbo *Sikala* tunapata jazanda ya **sigara. Angalia mshororo huu** :
*Ngwititye **sikala***
*Nimekuomba **sigara***

Katika mfano huu, ***sigara*** ni jazanda inayoashiria tendo la ngono. Katika wimbo huu, mhusika wa kiume anamwomba mhusika wa kike (Manguleti) sigara bila mafanikio. Neno sigara limetumika kijazanda na kitasfida kurejelea ngono na kuwasilisha umuhimu wa ubikira.

**Hitimisho**

Makala haya yamejadili uamilifu wa jazanda mbalimbali kama kipengee cha kifani na kimaudhui kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba. Utafiti huu umetambua kwamba jazanda kwenye nyimbo za kiasili za Kikamba zina dhima mahsusi kifani na kimaudhui. Jazanda huchangia katika kuchora taswira zinazorahisisha uelewa wa itikadi katika nyimbo za Kiasili za Kikamba. Jazanda pia hukuza na kutanua maana ya dhana. Vilevile, jazanda huimarisha kumbukumbu ya jumbe zinazowasilishwa pamoja na kuimarisha ujumi wa lugha. Kukuza taswira na hisia za hadhira, kusafidi lugha, kuzua utata wa kimaana kwa nia ya kuitenga hadhira pamoja na kukuza fikra za kiuhakiki miongoni mwa hadhira ni baadhi ya dhima za jazanda pia. Kwa hivyo, jazanda ni tamathali ya usemi yenye uamilifu mkubwa katika ujenzi wa fani na maudhui ya nyimbo za kiasili za Kikamba.

**Marejeleo**

Chun, L. (2003). *Cognitive Linguistics and Metaphor Studies*. Foreign Language Teaching and Research Press.
Honora, F., & Susan, S. (2012). *The reporter Who died Probing.* Amazon.
King'ei, K., & Kisovi, C. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi.* Kenya Literature Bureau.
Kovecses, Z. (2002). *Metaphor: A practical introduction*. Oxford University Press.
Kövecses, Z. (2003). Language, figurative thought and cross-cultural comparison. *Metaphor and Symbol*, 18(4), 311–320.
Lakoff, G., & Johnson, M. (1993). *The contemporary theory of metaphor.* https://escholarship.org/uc/item/54g7j6zh
Leech, G. N. (1969) *Linguistic Guide to English Poetry.* Longman.
Mbatia, M. (2000). *Mwanadamu na Hadithi Nyingine.* Jomo Kenyatta Foundation.
Nowottny, W. (1962) *The Language Poets Use.* The Athlone Press.
Okwena, S. (2013). *Matumizi ya Jazanda katika Tamthilia Tatu za Timothy Arege*. (Tasnifu ya cha Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta).
Richards, I. A. (1936). *The Philosophy of Rhetoric.* Oxford University Press.
Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Kauttu Limited.
Syambo, B. K., & Mazrui, A. M. (1999). *Uchambuzi wa Fasihi.* East African Educational Publishers.
TUKI. (2018). *Kamusi ya Kiswahili sanifu.* Oxford University Press.
Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia.* Focus Publishers.
Wamitila, K. W. (2008). *Kichocheo cha Fasihi. Simulizi na Andishi.* Press and Publicity Centre.